# TANZANIA BUSINESS LEADERS' PERCEPTIONS 2013





## Mazingira ya Uwekezaji nchini Tanzania

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy

## 1. UFUPISHO

Huu ni utafiti wa tano wa maoni ya wafanyabiashara Tanzania. Wafanyabiashara hao waliulizwa kuhusu:

*Mambo mbalimbali yanayosaidia mazingira wezeshi ya biashara;


• Mambo yanayoleta ugumu wa kufanya biashara
• Vizingiti vinavyosaidia kufanyika kwa biashara;
• Vizingiti vinavyosababisha ugumu wa kufanya biashara;
• Jinsi serikali inavyosaidia katika kuondoa vizingiti hivyo na;
• Tathmini ya gharama zinazohusika katika kutimiza matakwa ya sheria na urasimu.

Utafiti unaonyesha kwamba mambo yanayokwamisha uendeshaji na ukuaji wa biashara ni:

• Ukosefu wa umeme
• Kiwango cha kodi
• Rushwa
• Ulipaji wa kodi

Ukosefu wa umeme ni tatizo kubwa , likifuatiwa na barabara ingawa kwa mwaka 2012 barabara lilikuwa ni tatizo la sita. Kwa mwaka 2010, suala la upatikanaji wa maji halikuwa tatizo kubwa ingawa bado linaendelea kuonekana ni kikwazo kwa wafanyabiashara. Upatikanaji wa fedha, ambalo lilionekana ni tatizo mwaka 2009 na 2010, kwa mwaka 2011 kulikuwa na maendeleo mazuri ingawa mwaka 2012 hali ilikuwa mbaya.


Jedwali: Mambo yaliyochangia ugumu wa kufanya biashara kwa kuzingatia ukubwa wa tatizoO




Utafiti unataka kuonyesha iwapo serikali inafanya jitihada za kuyatafutia ufumbuzi matatizo haya. Ugumu wa kufanya biashara unaosababishwa na kila tatizo na jinsi serikali inavyofanya jitihada za makusudi kuyatafutia ufumbuzi matatizo hayo huunganishwa pamoja na kuwa kigezo kimoja cha 'mazingira wezeshi.'


Angalia katika jedwali ifuatayo kwamba namba ikiwa ndogo, ndivyo ukubwa wa kipaumbele ulivyo.

Jedwali 2: Kipaumbele cha mazingira wezeshi




Mambo ambayo serikali inatakiwa kuyapa kipaumbele yanaonyeshwa upande wa kulia wa jedwali namba 3, ambayo pia inaonyesha jinsi vipaumbele vilivyobadilika tangu 2008. Umeme na rushwa vinaendelea kuongoza katika orodha hiyo. Suala la kodi limejitokeza zaidi  -- hasa jinsi linavyotekelezwa – pia limejitokeza katika orodha hiyo.

Jedwali 3: Mabadiliko ya vipaumbele




Kutokuwepo kwa jambo lolote katika orodha hii hakuna maana kwamba serikali inaweza kupuuza, bali inatakiwa kufanya kila jitihada kupunguza vikwazo vinavyoathiri ukuaji wa biashara. Jitihada hizo ni lazima ziendelee ama sivyo hali hiyo itabidi iwe ni kipaumbele kwa siku zijazo. Lazima ieleweke wazi kwamba vigezo hivi ni vipimo linganishi tu na siyo vipimo mahsusi. Kwa hiyo tofauti kati ya kipimo linganishi kimoja na kingine ni ndogo mno.